

# Kifuatiliaji cha Urasimishaji:

Kutathmini ujumuishaji wa mpango wa elimu kwenye mfumo

## Kusudi

Zana hii husaidia kupima maendeleo ya juhudi za kurasimisha<sup>1</sup> au kuingiza mpango ndani ya mfumo rasmi wa elimu. Urasimishaji ni mbinu moja ya kuongeza matokeo katika elimu, ambayo pia hujulikana kama “upanuzi wa ngazi ya juu.” Ni mchakato unaotumika kufungamanisha mpango —au vipengele vya mpango<sup>2</sup>—ndani ya mfumo rasmi wa elimu na huongozwa na kudumishwa na wahusika wa serikali. Lengo kuu ni mpango kuwa sehemu ya sera, mipango, taratibu, bajeti na shughuli za kila siku za serikali; na hivyo katika hali bora zaidi, mpango huo haujitegemei au kupewa utambulisho wa pekee tena, bali “hutoweka” inavyofaa kwa kuingia ndani ya mfumo mpana, na hivyo kusaidia kuhakikisha uendeleu wake wa muda mrefu.

**Kutokana na hilo, zana hii inalenga kupima ujumuishaji wa mpango wa elimu katika mfumo uliopo wa elimu. Inakusudiwa kutumika kama zana ya mipango inayobadilishika kwa ajili ya watekelezaji, watunga sera na wafadhili ili kutambua na kushughulikia maeneo ambayo yanahitaji umakini wa ziada katika mchakato wa upanuzi katika ngazi za juu.**

Zana hii imepangwa kwa sehemu muhimu za mfumo wa elimu, ambazo zimegawanywa kwa vipengele maalum vya kila mojawapo. Kwa kila kipengele, kuna seti ya vigezo vya kuzingatia wakati wa kutoa alama, na safuwima ya kutoa maelezo ya alama iliyochaguliwa. Alama inatokana na kipimo cha 1–4, ambapo 1 inawakilisha “urasimishaji mdogo,” na 4 inawakilisha “urasimishaji kamili.” Ni muhimu kukumbuka kwamba kiasi cha maendeleo kinachohitajika ili kusonga mbele kutoka alama ya 3 hadi 4 kwa kawaida huwa kikubwa zaidi kuliko kusonga mbele kutoka 1 hadi 2.

Zana hii hupima maendeleo ya juhudi za urasimishaji zinazohusiana na shirika au wizara moja ya serikali, haswa wizara ya elimu (MoE). Hata hivyo, inawezekana kutumia zana hii kwa wizara tofauti ikiwa inafaa zaidi, ambayo inapaswa kubainishwa wakati wa kufafanua mawazo. Zana hii inakusudiwa kufuatilia maendeleo kuelekea urasimishaji katika ngazi ya kitaifa, lakini katika mfumo uliogatuliwa inaweza badala yake kufuatilia urasimishaji katika mamlaka husika za elimu za ngazi ya chini ya taifa. Ikumbukwe kwamba, zana hii haikusudiwa kubaini ikiwa mpango unapaswa kupanuliwa, au kutathmini uwezo wa mfumo wa elimu. Zana hii haifuatili vipengele vingine muhimu vya upanuzi, kama vile athari na ubora, na kwa hivyo kimsingi inapaswa kujaliziwa na vipimo vingine vya upanuzi. Hasa, inashauriwa kwamba zana hii inapaswa kuelekeza uundaji na/au urekebishaji wa mkakati mpana wa upanuzi na kutumika pamoja na nyenzo kama vile “Makala ya Mkakati wa Upanuzi” ya CUE.<sup>3</sup>

## Ushauri

Inashauriwa kwamba zana hii ijazwe kupitia majadiliano kati ya kundi la wadau muhimu wanaohusika katika mchakato wa upanuzi ambao wanaweza kufanya maamuzi na kuchukua hatua kulingana na matokeo ya zana. Mara nyingi hili huwa kundi dogo la msingi la watu kutoka shirika linalotekeleza, lakini pia linaweza kujumuisha wawakilishi kutoka wizara au idara ya serikali inayotarajiwa kutekeleza mpango huo katika kiwango kikubwa (yaani, taasisi tekelezi), shirika linalofadhili utekelezaji/upanuzi, na/au shirika mshenga (yaani, mhusika mwingine asiyeegemea upande wowote anayesaidia katika mchakato wa upanuzi). Kimsingi, kundi hilo la wadau linapaswa kutumia zana mara kwa mara (takribani kila baada ya miezi sita) kutathmini maendeleo na kubaini hatua za kuimarisha na kuendeleza juhudi za urasimishaji. Ikiwa mbinu hii haiwezekani katika mazingira maalum, zana inaweza pia kuandikwa na mtu na kisha kupeanwa kwa kundi kubwa la wadau kwa ajili ya majadiliano.

Zana hii inatokana na zana ya “Tathmini Urasimishaji wa Kifurushi cha Uingiliaji Kati” iliyotengenezwa na mpango mkuu wa Maternal and Child Survival Program (MCSP) wa United States Agency for International Development (USAID) ambao uliongozwa na Jhpiego, Management Systems International (MSI) na mtandao wa kimataifa wa ExpandNet na ambayo ilichapishwa kwa mara ya kwanza katika “Basic Toolkit for Systematic Scale Up.”<sup>4</sup> Imefanyiwa marekebisha na CUE katika Taasisi ya Brookings kwa ajili ya sekta ya elimu, kwa kutumia hoja kutoka kwa nyenzo mbalimbali ikiwemo mpango wa Mbinu ya Mifumo ya Matokeo Bora ya Elimu (Approach for Better Education Results, SABER) wa World Bank<sup>5</sup> na makala ya “sehemu 9 kuu za kujenga mfumo wa elimu wa kiwango cha kimataifa” ya National Center on Education and the Economy.<sup>6</sup>

# 1

## TAMBUA MAWAZO

- Je, lengo kuu ni kurasimisha vipengele vyote vya mpango ndani ya mfumo wa serikali, au baadhi ya vipengele tu? Ikiwa ni baadhi ya vipengele tu, ni vipengele vipi vinarasimishwa, ni vipi havirasimishwi, na ni kwa nini? Katika hali hii, neno “mpango” katika zana linawakilisha vipengele vinavyorasimishwa na si mpango “mzima”.
- Lengo kuu la urasimishaji na mpango kutolewa katika kiwango kikubwa ni lipi? Kufafanua maana ya urasimishaji kutaathiri moja kwa moja alama ambayo kila kipengele kinapewa.
- Wizara inayolengwa na juhudi za urasimishaji ni ipi na ni kwa nini? Je, zana inalenga urasimishaji katika ngazi ya kitaifa au ya chini ya taifa?

Zana (angalia ukurasa unaofuata) hujazwa kutoka safu hadi safu, ikiwezekana kupitia majadiliano na wadau wakuu. Kwa kila kipengele, kundi linakubaliana kuhusu hatua ya sasa ya urasimishaji (hupewa alama ya 1-4) na kujumuisha sentensi chache katika safuwima ya mwisho zinazoeleza ni kwa nini alama hii ilichaguliwa. Baadhi ya safu zinaweza kuhitaji kurekebisha kidogo ili kuendana vyema na hali halisi za mazingira ya eneo husika au mpango lengwa. Baadhi ya vipengele huenda pia visiwe vinahusika kulingana na mazingira na mpango lengwa; katika hali hii, acha kutoa alama na uandike “Haihusiki” katika safuwima ya mwisho. Ikiwa maendeleo ya kiwango cha sasa cha urasimishaji yako chini ya hali iliyoelezwa na alama ya “1,” chagua “1” na ujumuisha taarifa zaidi katika safuwima ya mwisho.

# 2

## PEA KILA KIPENGELE CHA URASIMISHAJI ALAMA

## 3 CHAMBUA MATOKEO

Matokeo ya zana yanaweza kuonyeshwa kwa muundo wa jedwali, au kama “chatu ya rada” au “grafu ya utando,” ili kuonyesha kwa mchoro maendeleo ya urasimishaji kwa kila kipengele ili kuwezesha majadiliano ya kundi (angalia Kiambatisho I kwa mfano). Kulinganisha matokeo ikiwa kuna mizunguko kadhaa ya data kunaweza kusaidia lakini si lazima, na chatu ya rada inaweza kusaidia hata kwa seti ya awali tu ya data. Onyesho la mchoro la matokeo ya zana linapaswa kusaidia kutambua maeneo ambapo maendeleo yanayotarajiwa hadi wakati husika yamefanyika na maeneo ambapo maendeleo yanakwama au yako katika hatua za awali.

## 4 BAINI VITENDO VYA KIPAUMBELE

Wadau muhimu wanapaswa kupitia na kujadili matokeo ili kubaini idadi ndogo ya maeneo ya kipaumbele ili kuendeleza mchakato wa urasimishaji (angalia sehemu ya “Baini vitendo vya kipaumbele” kwenye ukurasa wa 12 kwa maswali makuu ya kuzingatia). Lengo si lazima liwe kufikia alama ya “4” katika kila kipengele, bali kutambua vipengele vichache vya kipaumbele, kupanga mikakati ya jinsi ya kupiga hatua katika vipaumbele hivi, na kuainisha vitendo thabiti na vinavyowezekana vya kufanya ndani ya miezi sita hadi 12 ijayo ili kupiga hatua kuelekea urasimishaji mkubwa zaidi. Vitendo hivi muhimu na hatua zinazofuata zinapaswa kuingizwa katika mpango mpana wa upanuzi na mikakati wa mpango huo, kama ilivyotajwa hapo juu. Inawezekana kwamba wafanya maamuzi wakuu wenye mamlaka ya kuchukua hatua kutokana na matokeo ya zana hii huenda wasiwe wadau wale wale wanaohusika katika kuijaza; na katika hali hiyo, kuwasilisha na kushiriki matokeo ili kuchochea hatua ni sehemu muhimu ya hatua hii.

# Kifuatiliaji cha Urasimishaji

| SEHEMU MUHIMU YA MFUMO | KIPENGELE     | SWALI                                                                                                                                                  | URASIMISHAJI MDOGO                                                                                                                                                                                          |
|------------------------|---------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Mkakati wa upanuzi     | Maono na njia | Je, kuna maono na njia wazi ya kupanua mpango ndani ya MoE?                                                                                            | MoE ina nia ya kupanua mpango ndani ya mfumo wa elimu lakini bado haijaeleza maono au njia wazi.                                                                                                            |
|                        | Uongozi       | Je, kuna juhudi zinazoendelea za uongozi na uratibu kwa ajili ya mpango (mwanzoni na mtetezi/watetezi, na baadaye na kundi lililopangwa ndani ya MoE)? | Kuna angalau mtetezi au mratibu mmoja wa mpango katika MoE. Majadiliano yanaendelea na mtetezi/watetezi, ambaye anaweza kuunga mpango mkono katika mazungumzo ya ndani lakini bado si mtetezi wa hadharani. |
|                        |               | Je, mpango unaendana na sera zilizopo, au pale ambapo sera hazipo, je, MoE imetekeleza sera inayohitajika/zinazohitajika ili kuunga mkono mpango huo?  | Taasisi anzilishi inafanya majadiliano na MoE kuhusu kuendana kwa mpango na sera zilizopo.                                                                                                                  |
|                        |               | Je, MoE imejumuisha mpango katika mipango au mikakati ya kitaifa na ngazi za chini ya taifa?                                                           | Majadiliano yanaendelea na MoE ili kujumuisha mpango katika mpango/mipango au mkakati/mikakati ya kitaifa au ya ngazi za chini ya taifa.                                                                    |

**URASIMISHAJI  
UNAOIBUKA**

**URASIMISHAJI MKUBWA**

**URASIMISHAJI KAMILI**

**UFAPANUZI  
WA ALAMA  
ILIOCHAGULIWA**

**ALAMA = 2**

MoE inabuni maono ya kupanua mpango ndani ya mfumo uliopo na njia ya kufikia maono haya.

Mtetezi/watetezi au mratibu/waratibu huzungumza hadharani kuhusu mpango na kufanya juhudi za utetezi ili kuongeza kiasi cha uungwaji mkono ndani ya MoE kwa ajili ya upanuzi wa mpango.

Taasisi anzilishi na MoE wanarekebisha mpango ili uendane na sera husika zilizopo. Pale ambapo hazipo, sera zinazojumuisha mpango ziko katika mchakato wa kuundwa.

Majaribio ya mpango yamejumuishwa katika mpango/mipango au mkakati/mikakati ya ngazi za chini ya taifa.

**ALAMA = 3**

MoE imeweka maono na njia ya kupanua mpango ndani ya mfumo uliopo na kuwasilisha maono na njia hiyo kwa wafanya maamuzi wakuu.

Angalau afisa mmoja wa ngazi ya juu ndani ya MoE anaunga mkono mpango huo hadharani. Mtetezi/watetezi au mratibu/waratibu wanafanya juhudi za uhamasishaji kwa ajili ya mpango kujumuishwa katika mifumo iliyopo, ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa kupata ufadhili unaohitajika kwa kiwango cha kitaifa. Miundo inatengenezwa ili kusaidia kuratibu vipengele vya mpango katika mfumo mzima wa elimu.

Marekebisho ya mpango huo ili kuendana na sera zilizopo yanajaribiwa. Pale ambapo hazipo, sera zinazojumuisha mpango zinajaribiwa au kutekelezwa katika kiwango kidogo.

Mpango umejumuishwa katika mpango/mipango au mkakati/mikakati ya ngazi za chini ya taifa unakotekelezwa AU katika mpango/mipango au mkakati/mikakati ya kitaifa ya elimu lakini kwa sehemu ya nchi pekee.

**ALAMA = 4**

MoE imeelezea wazi maono ya kupanua mpango ndani ya mfumo uliopo na kuweka njia, mbinu na ratiba ya kufikia maono haya. Maono na njia vimewasilishwa katika ngazi zote muhimu za MoE. Kuna mchakato uliowekwa wa kupitia upya na kurekebisha njia hiyo/hizo mara kwa mara kama inavyohitajika.

MoE imetoa wafanyakazi wa kuwezesha usimamizi/udhibiti wa mpango ndani ya sehemu inayofaa ya MoE inayowajibika kwa utekelezaji na urasimishaji wake. Miundo imewekwa ili kuratibu vipengele vya mpango katika mfumo mzima wa elimu.

Mpango unaendana kikamilifu na sera zilizopo na/au sera zinazojumuisha mpango zimepitishwa na kutekelezwa.

Mpango umejumuishwa katika mpango/mipango au mkakati/mikakati ya kitaifa ya elimu.

# Kifuatiliaji cha Urasimishaji

| SEHEMU MUHIMU YA MFUMO |                                    | URASIMISHAJI MDOGO                                                                           |                                                                                                                                                                                                                               |
|------------------------|------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| KIPENGELE              |                                    | SWALI                                                                                        | ALAMA = 1                                                                                                                                                                                                                     |
| Rasilimali watu        | Wafanyakazi                        | Je, walimu wa serikali wanatekeleza mpango?                                                  | Majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu kuingiza utekelezaji wa mpango katika shughuli/maelezo ya kazi ya walimu wa serikali na mahitaji ya kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa.                 |
|                        | Kuajiri wafanyakazi na wafanyakazi | Je, kuna idadi ya kutosha ya walimu waliohitimu wa kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa? | MoE imebaini ni walimu wangapi wanaohitajika ili kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa na sifa za kitaalamu zinazohitajika lakini bado haina idadi ya kutosha.                                                             |
|                        | Mafunzo ya kazini                  | Je, mafunzo yanayofaa ya walimu ya kabla ya kazi ya MoE yanajumuisha mpango?                 | Taasisi anzilishi hutoa mafunzo yote yanayohusiana na mpango. Majadiliano yanaendelea ili kujumuisha mpango katika mafunzo yanayofaa ya kazini ya MoE.                                                                        |
|                        | Mafunzo ya kabla ya kazi           | Je, mafunzo yanayofaa ya walimu ya kabla ya kazi ya MoE yanajumuisha mpango?                 | Taasisi anzilishi hutoa mafunzo yote yanayohusiana na mpango. Majadiliano yanaendelea ili kujumuisha mpango katika mafunzo yanayofaa ya kabla ya kazi ya MoE.                                                                 |
|                        | Usimamizi na usaidizi              | Je, mpango umejumuishwa katika shughuli za kawaida za usimamizi na usaidizi za MoE?          | Taasisi anzilishi hufanya shughuli zote za usimamizi na usaidizi zinazohusiana na mpango. Marekebisho ya mfumo na nyenzo za usimamizi na usaidizi zilizopo za MoE yanaendelea ili kujumuisha mpango katika shughuli zilizopo. |

## URASIMISHAJI UNAOIBUKA

## URASIMISHAJI MKUBWA

## URASIMISHAJI KAMILI

UFAPANUZI  
WA ALAMA  
ILIYOCHAGULIWA

### ALAMA = 2

Walimu wameidhinishwa kutekeleza mpango na wanaanza kutekeleza vipengele vyake kwa usaidizi mkubwa kutoka kwa taasisi anzilishi.

### ALAMA = 3

Walimu wanatekeleza vipengele vya mpango, kwa usaidizi mdogo kutoka kwa taasisi anzilishi.

### ALAMA = 4

Walimu wanaongoza utekelezaji wa vipengele vyote vya mpango. Maelezo ya kazi yamepanuliwa ili kujumuisha shughuli zinazohusiana na mpango (ikiwa inahitajika) na MoE huweka matarajio wazi kwa walimu kuhusu mahitaji na matokeo yanayotarajiwa.

MoE inapanga na/au inaanza kufanya mchakato wa kuajiri wafanyakazi ili kuhakikisha kuna idadi ya kutosha ya walimu waliohitimu wa kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa.

Mchakato wa kuajiri wafanyakazi unaendelea kikamilifu. MoE inaweza kutoa idadi kubwa lakini isiyotosha ya walimu waliohitimu wa kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa.

MoE ina idadi ya kutosha ya walimu waliohitimu wa kutekeleza mpango katika kiwango kikubwa. Idadi hii hufadhiliwa ndani ya mfumo uliopo bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi, na kuna mpango wa kudumisha idadi inayohitajika.

MoE inasaidia taasisi anzilishi kutoa mafunzo ya kazini ya mpango lakini bado haijajumuisha mafunzo hayo katika mfumo uliopo.

Mpango umejumuishwa katika mafunzo ya kazini ya MoE, na MoE hutoa mafunzo kwa usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

Mpango umejumuishwa kikamilifu katika mafunzo ya kazini ya MoE, na MoE hutoa na kufadhili mafunzo bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

MoE inafanya majaribio ya kujumuisha mpango kwenye mafunzo ya kabla ya kazi, kwa usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

Mafunzo ya kabla ya kazi ya MoE yanajumuisha mpango, na MoE hutoa mafunzo kwa usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

Mpango umejumuishwa kikamilifu katika mafunzo ya kabla ya kazi ya MoE, na MoE hutoa na kufadhili mafunzo bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

Maafisa wa MoE wanaanza kufanya baadhi ya shughuli za usimamizi na usaidizi zinazohusiana na mpango, kwa usaidizi mkubwa kutoka kwa taasisi anzilishi.

Maafisa wa MoE na taasisi anzilishi hufanya shughuli za pamoja za usimamizi na usaidizi.

Miongozo ya usimamizi na usaidizi, mchakato na zana zinazohusiana na mpango zimejumuishwa na zinafadhiliwa kikamilifu ndani ya mfumo wa MoE. Usimamizi na usaidizi hufadhiliwa na kufanywa na MoE bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

# Kifuatiliaji cha Urasimishaji

| SEHEMU MUHIMU YA MFUMO | KIPENGELE                                | SWALI                                                                                                                                                                   | URASIMISHAJI MDOGO                                                                                                                                                                                                             |
|------------------------|------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Mtaala na vifaa        | Mtaala/viwango                           | <b>Je, mpango umejumuishwa katika mtaala/viwango vilivyopo vya MoE?</b>                                                                                                 | Mpango haujajumuishwa katika mtaala/viwango vya MoE vilivyopo, lakini majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu mahali na jinsi ya kuingiza mpango katika mtaala/viwango vilivyopo.                      |
|                        | Ununuzi wa vifaa na usambazaji           | <b>Je, MoE inaunda, inanunua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohitajika kwa kiasi na ubora wa kutosha kupitia mfumo wake wa kawaida wa ugavi?</b> | Taasisi anzilishi inawajibika kikamilifu kwa uundaji, ununuzi na usambazaji wa vifaa. Majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohitajika kwa ajili ya mpango. |
| Taarifa                | Usimamizi wa data                        | <b>Je, mpango umejumuishwa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Elimu (EMIS) au mfumo mbadala wa usimamizi wa data wa MoE uliopo?</b>                                | Taasisi anzilishi huendesha usimamizi wote wa data unaohusiana na mpango. Majadiliano yanaendelea kuhusu kujumuisha mpango katika EMIS au mfumo mbadala wa usimamizi wa data wa MoE uliopo.                                    |
|                        | Ufuatiliaji, tathmini na kujifunza (MEL) | <b>Je, MoE imefafanua na kutekeleza mkakati wa kufuatilia na kutathmini mpango na kutumia matokeo kurekebisha mpango?</b>                                               | Taasisi anzilishi hufanya MEL zote zinazohusiana na mpango. Majadiliano yanaendelea na MoE kuhusu kutengeneza mkakati wa MEL unaoweza kuendana na muundo wa MEL wa MoE.                                                        |
|                        | Tathmini ya wanafunzi                    | <b>Je, tathmini ya matokeo ya kujifunza yanayohusiana na mpango imejumuishwa katika tathmini rasmi za wanafunzi za MoE?</b>                                             | Taasisi anzilishi hufanya tathmini zote za matokeo ya kujifunza yanayohusiana na mpango. Majadiliano yanaendelea kuhusu kujumuisha tathmini ya utendaji wa wanafunzi unaohusiana na mpango katika tathmini zilizopo.           |

**URASIMISHAJI  
UNAOIBUKA**

**URASIMISHAJI MKUBWA**

**URASIMISHAJI KAMILI**

**UFAPANUZI  
WA ALAMA  
ILIYOCHAGULIWA**

**ALAMA = 2**

MoE imeandaa mpango na ratiba ya kujumuisha mpango katika mtaala/viwango vilivyopo. Marekebisho ya mtaala wa mpango yanafanyiwa majaribio, ikiwa yanafaa.

Wafanyakazi wa MoE waliopewa jukumu la kuwezesha mpango wametathmini mifumo ya kawaida ya ununuzi na usambazaji ili kubaini mahali ambapo vifaa vya mpango vinaweza kujumuishwa kwenye mifumo na michakato iliyopo.

MoE inapanga kujumuisha mpango katika EMIS au mfumo mbadala wa usimamizi wa data wa MoE uliopo. MoE inashirikiana na taasisi anzilishi ili kubaini hatua zinazofuata na ratiba ya kufanya marekebisho na kuchukua shughuli za usimamizi wa data.

MoE inapanga kujumuisha mkakati wa MEL unaohusiana na mpango kwenye miundo iliyopo na inashirikiana na taasisi anzilishi kuhusu kubuni mpango na ratiba ya utekelezaji wake.

MoE imeunda mpango na ratiba ya kuchukua umiliki wa tathmini ya matokeo ya kujifunza yanayohusiana na mpango na kuiweka ndani ya mfumo wake uliopo.

**ALAMA = 3**

Sera inaandaliwa ili kujumuisha mpango katika mtaala/viwango vilivyopo vya MoE.

Wafanyakazi wa MoE hutumia fedha za serikali kuunda, kununua na kusambaza vifaa kupitia mifumo iliyopo ya MoE. Taasisi anzilishi inachangia katika ufadhili, ununuzi na/au usambazaji wa vifaa.

MoE imejumuisha mpango katika EMIS au mfumo mbadala wa usimamizi wa data uliopo na imeanza kikamilifu kukusanya, kusimamia, kuchambua, kuhifadhi na kutumia data kwa usaidizi kiasi kutoka kwa taasisi anzilishi.

MoE imejumuisha mkakati wa MEL unaohusiana na mpango katika utaratibu wake wa MEL na mara kwa mara hutumia matokeo yake kuboresha muundo na uendeshaji wa mpango, lakini shughuli za MEL zinazohusiana na mpango mara chache hupokea usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

MoE hufanya tathmini ya matokeo ya kujifunza yanayohusiana na mpango—kwa usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi—lakini hii bado haijajumuishwa katika tathmini zilizopo.

**ALAMA = 4**

Mpango umejumuishwa kikamilifu katika mtaala/viwango rasmi. MoE inawajibika kikamilifu kufanya marekebisho ya mtaala.

Uundaji, ununuzi na usambazaji wa vifaa bora vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia vinavyohusiana na mpango unafadhiliwa kikamilifu na serikali na umejumuishwa katika mifumo ya MoE (utabiri, ugavi, usambazaji na usimamizi).

MoE hufanya yenyewe shughuli zote za usimamizi wa data zinazohusiana na mpango bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi; mpango umejumuishwa kikamilifu katika EMIS au mfumo mbadala wa usimamizi wa data uliopo.

MoE hufuatilia na kutathmini shughuli na athari za mpango ndani ya taratibu zilizopo na hutumia matokeo hayo kuboresha miundo na uendeshaji, bila usaidizi wowote kutoka kwa taasisi anzilishi.

Matokeo ya kujifunza yanayohusiana na mpango hutathminiwa kama sehemu ya tathmini rasmi za wanafunzi za MoE. Taasisi anzilishi haishiriki vyovyote katika tathmini za wanafunzi.

# Kifuatiliaji cha Urasimishaji

| SEHEMU MUHIMU YA MFUMO | KIPENGELE                  | SWALI                                                                                                                                                      | URASIMISHAJI MDOGO                                                                                                                                                                                                                                                                                                               |
|------------------------|----------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| Fedha                  | Fedha                      | Je, vipengele vyote vya utekelezaji wa mpango vinafadhiliwa na serikali?                                                                                   | Taasisi anzilishi na/au wafadhili wa nje hufadhili gharama zote zinazohusiana na mpango lakini majadiliano yanaendelea na MoE kuhusu serikali kutoa fedha moja kwa moja au msaada wa aina nyingine.                                                                                                                              |
|                        | Ushiriki wa wadau          | Je, MoE inashiriki katika kuzalisha hitaji na uungwaji mkono wa mpango miongoni mwa wanufaishwa watarajiwa na wadau muhimu katika mfumo ikolojia wa elimu? | Taasisi anzilishi hufanya shughuli zote za kuzalisha hitaji na ushiriki. Majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu mikakati ya kuzalisha hitaji na uungwaji mkono miongoni mwa wanufaishwa watarajiwa na wadau muhimu.                                                                                     |
| Ushiriki wa wadau      | Uzalishaji wa hitaji       | Je, MoE inatambua na kuzungumza na wapinzani watarajiwa wa upanuzi na wale ambao wanaweza kupata hasara fulani kutokana na kuenea kwa mpango?              | MoE kwa usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi inashughulika ili kubaini wapinzani watarajiwa wa upanuzi na wale ambao wanaweza kupata hasara fulani kutokana na upanuzi wa mpango.                                                                                                                                               |
|                        | Upinzani                   | Je, MoE imehakikisha kuwa wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu watapata ufikiaji sawa wa mpango?                                         | MoE haijachukua hatua ili kushughulikia mahitaji mahususi ya wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu ili kuhakikisha ufikiaji sawa wa mpango. Majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu vikwazo vinavyoweza kuwazuia wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu kufikia mpango. |
| Usawa na ujumuishaji   | Ufikiaji sawa na jumuiishi | Je, MoE imehakikisha kuwa wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu watapata ufikiaji sawa wa mpango?                                         | MoE haijachukua hatua ili kushughulikia mahitaji mahususi ya wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu ili kuhakikisha ufikiaji sawa wa mpango. Majadiliano yanaendelea kati ya MoE na taasisi anzilishi kuhusu vikwazo vinavyoweza kuwazuia wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu kufikia mpango. |

## URASIMISHAJI UNAOIBUKA

## URASIMISHAJI MKUBWA

## URASIMISHAJI KAMILI

UFAPANUZI  
WA ALAMA  
ILIOCHAGULIWA

### ALAMA = 2

Taasisi anzilishi na/au wafadhili wa nje hufadhili upanuzi wa mpango. Serikali hutoa ufadhili kiasi (kupitia gharama za moja kwa moja na/au msaada wa aina nyingine), na inaandaa mpango wa kupunguza ufadhili wa nje hadi kufikia sifuri kadri muda unavyopita.

### ALAMA = 3

Serikali hufadhili angalau nusu ya gharama zote zinazohusiana na mpango na inashughulika ili kupunguza zaidi ufadhili wa nje kadri muda unavyopita lakini inapokea usaidizi wa nje unaoendelea.

### ALAMA = 4

Serikali hugharamia gharama zote zinazohusiana na mpango, na mpango umejumuishwa katika bajeti ya serikali.

Taasisi anzilishi huongoza shughuli za uzalishaji wa hitaji na ushiriki, kwa usaidizi usio rasmi kwa mchakato huo kutoka kwa angalau mfanyakazi mmoja wa MoE, ikiwa ni pamoja na kutambua njia za kuzalisha hitaji na kujenga uungwaji mkono kupitia njia zilizopo za MoE.

Shughuli za kuzalisha hitaji na ushiriki ni sehemu rasmi ya mpango kazi wa MoE, na MoE inaongoza shughuli zinazohusiana na kuzalisha hitaji na uungwaji mkono miongoni mwa wanufaishwa watarajiwa na wadau muhimu kwa usaidizi unaoendelea kutoka kwa taasisi anzilishi.

MoE inaongoza shughuli zote zinazohusiana na uzalishaji wa hitaji na uungwaji mkono bila usaidizi kutoka kwa taasisi anzilishi.

MoE inaandaa mpango wa kuzungumza na wapinzani watarajiwa wa upanuzi na wale wanaoweza kupata hasara fulani, ili kuelewa vyema na kushughulikia wasiwasi wao na/au kupunguza upinzani wao.

MoE inatekeleza mpango wa kuzungumza na wapinzani watarajiwa wa upanuzi na wale wanaoweza kupata hasara fulani, ili kushughulikia wasiwasi wao na/au kupunguza upinzani wao kwa njia chanya.

MoE inashirikiana kikamilifu na wapinzani watarajiwa wa upanuzi na wale ambao wanaweza kupata hasara fulani, ikijitahidi kushughulikia wasiwasi wao na/au kupunguza uwezekano wao wa kuwa chanzo cha usumbufu katika upanuzi.

MoE imefanya uchambuzi ili kubaini mahitaji mahususi ya wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu au imepokea uchambuzi uliofanywa na taasisi anzilishi lakini bado haijachukua hatua ili kuhakikisha ufikiaji sawa wa mpango.

MoE imeunda mkakati wa kuhakikisha ufikiaji sawa wa mpango kwa wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu na imeanza utekelezaji katika baadhi ya maeneo ya majaribio.

MoE imetekeleza mkakati katika ngazi ya kitaifa ili kutoa ufikiaji sawa wa mpango kwa wanafunzi waliotengwa na walio katika mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na kutoa rasilimali zaidi za watu na/au fedha, na ina mbinu za uwajibikaji zilizowekwa ili kufuatilia jinsi wanafunzi hawa wanavyohudumiwa.

## Baini vitendo vya kipaumbele

**Vipengele vichache vya kipaumbele kwa miezi 6–12 ijayo ni vipi?**


**Ni vitendo gani thabiti vinavyohitajika ili kupiga hatua kwa kila kipengele?**

**Kufikia lini?**

**Ni nani ataongoza?**

## Kiambatisho I: Mfano wa grafu ya rada

Njia moja ya kuonyesha matokeo ya Kifuatiliaji cha Urasimishaji kwa michoro ni kupitia grafu ya rada au utando. Aina hii ya chati inaweza kuwezesha majadiliano kuhusu vipengele vya urasimishaji vinavyopaswa kupewa kipaumbele kama hatua za utekelezaji katika siku zinazofuata na pia kuonyesha kwa vilelezo maendeleo katika matumizi mbalimbali ya zana. Hapa chini kuna mfano wa grafu ya rada inayoonyesha matokeo ya mizunguko miwili.



# Marejeleo

1. Mfumo wa Upanuzi wa Expandnet hutumia ufafanuzi ufuatao: "Urasimishaji (sera, kisiasa, kisheria au upanuzi wa ngazi ya juu) ni ujumuishaji wa uvumbuzi katika sera, miundo na miongozo ya utendaji." Angalia: <https://expandnet.net/scaling-upframework-and-principles/>
2. Neno "mpango" katika zana hii linaweza kutumika kurejelea programu ya elimu, mfumo au sera nzima au vipengele mahususi vya mfumo au mbinu. Ni muhimu kubainisha maana ya mpango kwa kundi mahususi linalojaza zana mwanzoni mwa mchakato, ili kuwe na uwazi wakati wote wa kuchagua alama.
3. Jenny Perlman Robinson, Molly Curtiss Wyss na Patrick Hannahan, "Scaling Strategy Worksheet: Planning for Scale," (Washington DC: Brookings Institution, Julai 2021).
4. Taasisi anzilishi huunda na kufanya majaribio ya mpango wa awali wa elimu, iwe ni mfumo, mbinu au mfano wa awali, nk. na taasisi tekelezi huchukua na kutekeleza mfumo huo katika kiwango kikubwa. Hapa neno "taasisi" linaweza kurejelea shirika, taasisi, wakala au idara ya serikali au isiyo ya serikali. Angalia: Ruth Simmons na Jeremy Shiffman, "Scaling-up Reproductive Health Service Innovations: A Conceptual Framework," makala iliyoandaliwa kwa ajili ya Mkutano wa Bellagio: Kutoka Miradi ya Majaribio hadi Sera na Mipango (From Pilot Projects to Policies and Programs) (2003).
5. Imetolewa kwenye Zana ya 11: Tathmini Urasimishaji wa Kifurushi cha Mpango katika "Mkusanyiko wa Zana za Msingi za Upanuzi wa Kimfumo: Toleo Rejea la Mwongozo wa Mratibu wa Upanuzi la Kuwezesha Juhudi Zinazoongozwa na Nchi za Kupanua na Kudumisha Kimfumo Mipango ya Afya ya Uzazi, Mama, Watoto Wachanga, Watoto na Vijana," (Juni 2019). Mwongozo na mkusanyiko huo wa zana vilitengenezwa kwa ushirikiano kati ya mpango mkuu wa Maternal and Child Survival Program (MCSP) wa United States Agency for International Development (USAID) na mtandao wa kimataifa wa ExpandNet, <https://www.mcsprogram.org/wp-content/uploads/2020/03/Basic-Toolkit-for-Systematic-Scale-Up.pdf>.
6. <http://saber.worldbank.org/index.cfm>.
7. Marc Tucker, "Vigae 9 vya Mfumo wa Elimu wa Kiwango cha Dunia," (Washington, DC: Kituo cha Kitaifa cha Elimu na Uchumi, 2016).
8. Katika zana hii, CUE hutumia neno mwalimu kujumuisha walimu, pamoja na watu wengine waliopewa jukumu la kutekeleza mpango wa elimu, kama vile wakufunzi wa walimu, makocha, washauri, wawezeshaji wa vijijini na aina nyingine za waelimishaji. Wafanyakazi wanaohitajika wanaweza kubainishwa katika jedwali la mawazo unapoanza kutumia zana.

## Kifuatiliaji cha Urasimishaji

2026

Zana hii ilitengenezwa na Jenny Perlman Robinson, Molly Curtiss Wyss na Patrick Hannahan, pamoja na michango kutoka kwa washirika wetu wengi wa Real-time Scaling Lab, wanachama wa Kikundi cha Ushauri, wanagenzi na wafanyakazi wenza wengine.

Pia tunatoa shukrani zetu kwa Katie Portnoy na Esther Rosen kwa usaidizi wao wa uhariri na usanifu. Ili kushiriki uzoefu wako wa kutumia zana hii au kutoa maoni yoyote kwa ajili ya matoleo yajayo, tafadhali tuma barua pepe kwa [CUE@brookings.edu](mailto:CUE@brookings.edu).

Zana hii ni sehemu ya mfululizo kuhusu upanuzi unaowezeshwa na usaidizi kutoka kwa Wakfu wa Bernard van Leer, Wakfu wa BHP, ELMA Philanthropies, Inc. kupitia Kampeni ya Elimu ya Wanawake (CAMFED), Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa, Kanada kupitia Wakfu wa Elimu na Maendeleo ya Teknolojia ya Habari (FIT-ED), Kamati ya Uokoaji ya Kimataifa na Wakfu wa Jacobs. Maoni yaliyotolewa katika zana hii ni ya waandishi wake na hayawakilishi maoni ya wafadhili, maafisa wao, wafanyakazi au Bodi za Magavana.